# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA HAMSINI NA MOJA

**23 JUNI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA HAMSINI NA MOJA - TAREHE 23 JUNI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI MKUU:**

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**648 MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mkakati upi katika kusimamia na kutoa msaada wa kisaikolojia kwa Watu wenye Ulemavu.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

### 649 MHESHIMIWA BAHATI KENETH NDINGO (MBARALI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kukarabati Barabara ya Igalako – Mwatenga hadi Mapala Mbarali.

### 650 MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA (KILINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Daraja la Sambu katika Kata ya Masagalu - Kilindi.

### 651 MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni utaratibu gani unatumika kugawa miradi ya kimkakati katika maeneo mbalimbali nchini.

**652 MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuigawa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ili kurahisisha shughuli za kiutawala.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**653 MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuratibu zoezi la Walimu kuhama Vituo vya kazi hasa maeneo ya Vijijini kwenda Mijini.

**WIZARA YA NISHATI:**

**654 MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHALWE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha kusambaza umeme Nkangamo – Momba.

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

**655 MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali imejipangaje kusaidia Wahanga wanaopata mimba kutokana na ukatili wa kijinsia wa mashambulio ya kingono na ubakaji.

**656 MHESHIMIWA TAMIMA HAJI ABASS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, kuna mpango gani wa kuyapatia Madawati ya Jinsia nchini vitendea kazi ikiwemo magari.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**657 MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kuna mpango gani wa kutengeneza miundombinu ya kisasa katika Gereza la Sumbawanga.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

### 658 MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mnada wa Mifugo wa Kintinku katika Halmashauri ya Manyoni.

## WIZARA YA MAJI:

### 659 MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA (NEWALA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itajenga miundombinu katika visima viwili vya maji Vijiji vya Mpalu na Lochinu ili kuondoa adha ya maji.

## WIZARA YA UJENZI:

### 660 MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MASWA MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Maswa kupitia Shishiyu - Malya hadi Nyambiti Mwanza.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**661 MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga upya Kiwanja cha Michezo katika Chuo na Shule ya Mahitaji Maalum Patandi.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **23 JUNI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |